Idara ya Haki ya Marekani
Shirikisho la Upelelezi la FBI

# MWONGOZO WA KIITIKIO CHA TISHIO NA OGOFYA

## TISHIO LA ANA KWA ANA

**TISHIO LA ANA KWA ANA LA KIMWILI ni wakati uko katika hatari ya karibu kwa sababu ya ukaribu wako na mtu yule anayefanya tishio. Uko na chaguo tatu:**

1. **Kimbia:** Tambua njia ya kutoroka. Wacha vifaa vyovyote ambavyo vinaweza kukupunguzia mwendo, saidia wengine kutoroka. Piga simu 911.
2. **Jifiche:** Jifiche mbali na mandhari ya tishio. Funga milango au zuia viingilio. Nyamazisha simu yako ya rukono (pamoja na mtikisiko) na kaa kimya hadi tishio hilo liishe.
3. **Fanya Vita:** Kufanya vita kunapaswa kuwa hatua ya mwisho na kama tu maisha yako yapo katika hatari ya karibu. Jaribu kuondolea tishio hilo nguvu. Tenda kwa jeuri ya kimwili kwa kadiri iwezekanavyo.

**TISHIO LA ANA KWA ANA LA MANENO ambalo halimuweki mpokeaji wa tishio hilo katika hatari ya karibu au linakusudiwa kutekelezwa baadaye.**

- Andika au vinginevyo rekodi tishio haswa kama lilivyowasilishwa.
- Rekodi maelezo ya kuainisha mengi iwezekanavyo juu ya mtu aliyefanya tishio: jina, umbo, rangi ya ngozi, jinsia, urefu, uzito, rangi ya nywele na macho, sauti, mavazi, au maumbile mengine yoyote ya kutofautisha.
- Piga ripoti la tishio hilo kwa watekelezaji wa sheria.

## TISHIO LA SIMU

**TISHIO LA SIMU ni tishio ambalo limepokewa kupitia simu. Unapaswa kujaribu kupata habari nyingi iwezekanavyo juu ya mpigaji simu na tishio, isipokuwa hilo tishio liko karibu au linaweza kukudhuru wewe au wengine kwa upesi.**

- Kaa mtulivu na usikate simu.
- Mweke mpigaji kwenye simu kwa muda mrefu iwezekanavyo na jaribu kuomba habari ili kuamua kama tishio hilo ni la namna yake, halisi, au linaleta hatari ya karibu kwako au kwa wengine.
- Ikiwezekana, ashiria wengine waliokaribu wasikilize na wajulishe watelekezaji wa sheria.
- Nakili habari yoyote iliyo katika onyesho la elektroniki la simu.
- Andika maneno haswa ya tishio.
- Rekodi simu ikiwezekana.
- Kuwa tayari kujadili maelezo na watumishi wa sheria.

## TISHIO LA UJUMBE WA ELEKTRONIKI

**TISHIO LA UJUMBE WA ELEKTRONIKI ni tishio ambalo linapokewa kupitia ujumbe wa moja kwa moja, barua pepe, au mtandao wa kijamii. Yaweza husisha tishio za mlungula au matokeo mabaya mpokeaji akikosa kutii.**

- Usifunguwe ujumbe wa elektroniki au kiambatisho kutoka kwa watumaji wasiojulikana.
- Usiwasiliane kupitia mtandao wa kijamii na watu usiofahamu au watu ambao hujaomba mawasiliano.
- Hakikisha mipangilio yako ya usalama imewekwa katika kiwango cha ulinzi cha juu.

**Kama tishio la elektroniki limepokewa:**

- Usifute ujumbe huo. Uchunguzi wa kisheria waweza kufichua maelezo muhimu.
- Acha ujumbe wazi katika tarakilishi.
- Julisha watekelezaji wa sheria mara moja.
- Chapisha, piga picha, au nakili ujumbe huo, mstari wa mada, tarehe, na saa.
- Hifadhi ushahidi wote wa elektroniki.

## MASHAMBULIZI YA MTANDAO

**SHAMBULIZI LA MTANDAO laweza kuhatarisha kifaa chako cha elektroniki na fichua habari za kibinafsi.**

- Tumia maneno siri imara na usitumie neno siri sawa katika tovuti mbalimbali.
- Weka kinga dhidi ya virusi na programu hasidi ili zijisasishe kwa kujiendesha.
- Tumia masasisho ya mifumo na programu mara tu yanapopatikana.
- Tumia hatua mbili za uthibitisho.
- Rejesha data mara kwa mara.

**Ukishuku kwamba umekuwa mwathirika wa shambulizi la mtandao:**

- Usifute au kubadilisha mifumo ya tarakilishi yako.
- Wasiliana mara moja na taasisi zako za fedha kuhifadhi akaunti zako dhidi ya wizi wa utambulisho.
- Badilisha maneno siri na fuatilia akaunti kwa shughuli zenye kutuhumu.

***Kama uko kwa hatari ya kimwili ya karibu, piga simu 911***
*Ukipata tishio, tafadhali wasiliana na ofisi ya FBI ya mtaa wako (orodha zinapatikana katika www.fbi.gov)*

***Unaweza pia fanya kidokezo kisichojulikana kwa FBI kupitia simu au mtandao.***

Idara ya Haki ya Marekani
Shirikisho la Upelelezi la FBI

# MWONGOZO WA KIITIKIO CHA TISHIO NA OGOFYA

## Ninapaswa kuwasiliana na nani nipatapo tishio au ogofya: polisi wa mtaa au FBI?

- Kama wewe au wengine mko katika hatari ya kimwili ya karibu, pigia polisi wa mtaa kwa kupiga 911.
- Ukipata tishio linalohusiana na jinai ya shirikisho, wasiliana na ofisi ya FBI ya mtaa wako (orodha ziko katika www.fbi.gov) kwa kupiga 1-800-CALLFBI (au 1-800-225-5324) au kupitia www.fbi.gov/tips. Mifano ikiwemo tishio kutoka kwa wakala wa serikali ya kigeni, jinai iliyopangwa, au afisa wa serikali. Ripoti yako inaweza kuwa bila jina.
- Sio matukio yote yanoyokidhi kizingiti cha upelelezi wa FBI. Ukiwa mwathirika wa tukio ambalo halikidhi kizingiti cha jinai ya shirikisho, utahitaji kuripoti hilo tukio kwa idara ya polisi ya mtaa wako. Mamlaka ya mitaa na majimbo ina vizingiti tofauti vya kupeleleza jinai za kushukiwa.

## Naweza kutarajia nini nikihojiwa na FBI?

- Wakala wa FBI anaweza kukutana nawe katika ofisi ya mtaa ya FBI au katika eneo lingine .
- FBI watakuuliza uwape habari nyingi iwezekanavyo kuhusu huyo mhalifu na maelezo ya tishio ulilopata.
- FBI watakuitisha maelezo ya mawasiliano yako ili wafuatilie nawe ikihitajika.
- FBI watajitahidi kuhifadhi utambulisho na usiri wako.
- Ikiwa inafaa, Mtaalamu wa Waathirika wa FBI anaweza kuwemo wakati wa mahojiano ili kukupa maelezo na usaidizi, au wanaweza kuwasiliana nawe baada ya mahojiano kupitia simu au barua.

## Ni kizingiti kipi ambapo FBI watapeleleza mashtaka na/au kuanza upelelezi?

- FBI wanaweza kuchunguza matishio yanayovunja sheria za shirikisho la Marekani na vinavyoashiria madhara au hatari kwa mpokeaji.
- Uwezo wa Serikali ya Marekani kuwashtaki watu binafsi kwa mashtaka yanayohusiana na matishio hutegemea mambo kadhaa, kama vile: ubora wa ushahidi, uwezo wa kuwatambua watu waliotekeleza kitendo hicho, utambulisho wa njama, na/au uwezo wa kuwafunga wahalifu hao.

## Nitatarajia nini FBI wakianza ulepelezi?

- FBI ikiamini kuwa kunauwezo jinai la shirikisho limetendwa, wakala wa FBI mmoja au zaidi watafanya upelelezi. Ndani ya upelelezi huo, wakala maalum watakusanya ushahidi, ambao unaweza kujumuisha mahojiano na wewe na waathirika wengine.
- Unaweza pia kuombwa uelezee tajiriba yako mbele ya baraza la waamuzi kuu la shirikisho.
- Upelelezi mkamilifu utatimilizwa. Upelelezi unaweza kuchukua muda mrefu kutimiza, na hautajulishwa maendeleo ya kesi ya siku kwa siku. Kila jitihada itafanywa kukujulisha juu ya matukio muhimu katika upelelezi, kama kukamatwa au shtaka rasmi lililoandikwa. FBI imejitolea kukupatia habari hio kabla haijatolewa kwa umma. Hata hivyo, lazima FBI wawe makini wasifichue habari nyeti ambayo inaweza kudhuru upelelezi au hatarisha zaidi watekelezaji wa sheria .
- Mtaalamu wa Waathirika wa FBI atakuwepo kuwapa waathirika waliotambuliwa usaidizi, habari, na kuwaelekeza kwa rasilimali zozote katika mtaa ambazo zinaweza hitajika.

***Hata kama kuripoti maelezo ya vile ulivyotishwa au kuogofishwa haitatokeza upelelezi, itayamkini saidia waathirika wengine kwa kusaidia FBI kufuatilia matishio na kutambua maelekeo.***

***MAELEZO YA MAWASILIANO YALIYO ORODHESHWA KWA MIJI NA MAJIMBO YANAPATIKANA KATIKA WWW.FBI.GOV. KAMA UKO KATIKA HATARI YA KARIBU, PIGA 911.***